JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

KITABU CHA MIRADI YA MAENDELEO INAYO WEKWA MAWE YA MSINGI NA INAYOZINDULIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU TAREHE 10-04-2017

SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NCHI YETU

Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 229
Sumbawanga

10 APRILI 2017

NA	YALIYOMO	UKURASA
1.	Ramani ya Mbio za Mwenge wa Uhuru tarehe 10 Aprili 2017	3
2.	Ratiba ya Mbio za Mwenge wa uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	4-8
3.	Wakimbiza mwenge kitaifa	8
4	Taarifa fupi ya mradi wa ufugaji Nyuki kijiji cha Kizungu	9
5.	Taarifa fupi ya mradi wa ujenzi wa nyumba bora ya mwananchi kijiji cha Muze	10
6	Taarifa fupi ya mradi wa ujenzi wa Jengo la Utawala shule ya Sekondari Vuma	11
7	Taarifa fupi ya mradi wa ujenzi wa chumba kimoja cha Maabara katika Sekondari ya Vuma	12
8	Taaarifa fupi ya uhawilishaji wa Ruzuku kwa Kaya Masikini chini ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) kijiji cha Mtowisa 'A'	13
9	Taarifa fupi ya kukabidhi Mikopo kwa vikundi vya Vijana na Wanawake	14
10	Taarifa fupi ya Mkulima wa zao la Alizeti kijiji cha Zimba	15
11	Taarifa fupi ya Ujenzi wa Nyumba ya Walimu 6 (six in one) Shule ya Sekondari Milenia	16
12	Taarifa fupi ya Klabu ya Wapinga Rushwa na Madawa ya Kulevya shule ya Sekondari Milenia	17
13	Taarifa fupi ya mradi wa ujenzi wa Vyumba viwili vya madarasa Shule ya Sekondari Milenia	18
14	Taarifa fupi ya Mradi wa Ufugaji wa Samaki kijiji cha Milepa	19
15	Taarifa fupi ya mradi wa Ujenzi wa Zahanati kijiji cha Kinambo	20
16	Taarifa fupi ya mradi wa Maji kijiji cha Solola	21
17	Taarifa fupi ya ugawaji wa Vyandarua Ilemba	22
18	Taarifa fupi ya Kukabidhi zawadi kwa Shule za Msingi na Sekondari zilizofanya vizuri katika Mtihani mwaka 2016	23
19	Mhutasari wa thamani ya Miradi ya maendeleo itakayopitiwa na Mbio za Mwenge mwaka 2017	24-25

RAMANI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU
TAREHE 10-4-2017



RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017 KUANZIA TAREHE 10/04/2017 HADI TAREHE 11/04/2017

TAREHE	MUDA	SHUGHULI	MAHALI	KM	MHUSIKA
10/4/2017	2:00 - 3:00	Wananchi,vikundi vya burudani kuwasili na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kufanya maandalizi ya kuupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga	Kijiji cha Kizungu	0	DC Sumbawanga , Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya Sumbawanga
	3:00 - 3:20	Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	Kijiji cha Kizungu	0	DC Sumbawanga na DED Sumbawanga
	3:20 - 3:30	DC Sumbawanga Kumkabidhi Mwenge DED Sumbawanga	Kijiji cha Kizungu	0	DC Sumbawanga , DED Sumbawanga
	3:30 - 3:35	Kukabidhi Mizinga kumi (10) ya Nyuki kwa Kikundi cha wafugaji wa Nyuki kijiji cha Kizungu na kukabidhi jozi tano (5) za Kurinia Asali kwa Vikundi kutoka Mfinga na Muze	Kijiji cha Kizungu	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	3:35 - 3:50	Mwenge Kuondoka Kizungu na kuwasili Muze	Muze	13	DC Sumbawanga , OCD
	3:50 - 3:55	Kuweka jiwe la Msingi ujenzi wa Nyumba Bora ya Mwananchi	Muze	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	3:55 - 4:25	**UJUMBE WA MWENGE** (Stand ya Muze)	Muze	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge

	4:25 - 4:30	Mwenge kuondoka Muze (Stand) na kuelekea eneo la Chai ukumbi wa Muze	Muze	0.7	DC Sumbawanga , OCD
	4:30 - 5:00	**CHAI** (Ukumbi wa Muze)	Muze	0	DC Sumbawanga , DED Sumbawanga
	5:00– 5:50	Mwenge kuondoka Muze kuelekea Mtowisa-Vuma Sekondari	Mtowisa	28	DC Sumbawanga , OCD
	5:50 -5:55	Kuzindua Maabara ya Kemia Shule ya Sekondari Vuma.	Mtowisa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	5:55 - 6:00	Kuweka jiwe la Msingi jengo la Utawala Sekondari ya Vuma	Mtowisa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	6:00 - 6:05	Mwenge kuondoka Vuma Sekondari na kuwasili kiwanja cha Mpira Shule ya Msingi Mtowisa.	Mtowisa	0.6	DC Sumbawanga , OCD
	6:05 - 6:10	Kutoa Vyeti kwa wanufaika wa TASAF (Waliofanya Vizuri)	Mtowisa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	6:10 - 6:15	Kukabidhi hundi ya mkopo kwa Vikundi viwili vya Vijana na Wanawake	Mtowisa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	6:15 - 6:40	**UJUMBE WA MWENGE** (Utafanyika Viwanja vya Shule Msingi Mtowisa)	Mtowisa	0	DC Sumbawanga , DED Sumbawanga
	6:40 - 6:55	Mwenge kuondoka Mtowisa kuelekea Zimba	Mtowisa	13	DC Sumbawanga , OCD
	6:55 -7:00	Kutembelea Shamba la Alizeti Kijiji cha Zimba	Zimba	0	Kiongozi wa Mbio za Mwenge
	7:00– 7:40	Mwenge kuondoka Zimba kupitia Msia, Talanda,Kisa **(Kushangilia Mwenge)** na kuwasili Milepa	Milepa	23	DC Sumbawanga . OCD

	7:40– 7:45	Kuweka jiwe la Msingi ujenzi wa Nyumba za Walimu **(SEDP - II)** Shule ya Sekondari Milenia	Milepa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	7:45–7:50	Kuzindua kikundi cha kupinga kutumia na kusambaza Madawa ya kulevya na kupambana na Rushwa, Shule ya Sekondari Milenia	Milepa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	7:50– 7:55	Kuweka Jiwe la Msingi Madarasa 2 **(SEDP – II)** Shule ya Sekondari Milenia	Milepa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	7:55 -8:35	**CHAKULA cha Mchana** (Milenia Sekondari)	Milepa	0	DC Sumbawanga na DED Sumbawanga
	8:35 -8:45	Mwenge kuondoka Shule ya Sekondari Milenia na kuwasili eneo la Bwawa la Samaki	Milepa	1	DC Sumbawanga , OCD
	8:45 - 8:50	Kuzindua Bwawa la Samaki Milepa	Milepa	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	8:50 - 9:15	Mwenge kuondoka Milepa na kuwasili Kinambo	Milepa	8	DC Sumbwanga, OCD
	9:15 - 9:20	Kuweka jiwe la Msingi ujenzi wa Zahanati ya Kinambo	Kinambo	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	9:20 - 9:40	Mwenge kuondoka Kinambo kupitia Mahenje, Lyanza, Sakalilo, Ilemba (**Kushangilia Mwenge**) na kuwasili Solola	Kinambo	20.6	DC Sumbawanga , OCD
	9:40- 9:45	Kuzindua Mradi wa Maji katika kijiji cha Solola	Solola	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	9:45- 9:50	Mwenge kuondoka kijiji cha Solola na kuwasili	Solola	1.1	DC Sumbawanga

		Ilemba			, OCD
	9:50-9:55	Kukabidhi Vyandarua 300 kwa akina mama wajawazito, Watoto na Wazee	Ilemba	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	9:55-10:05	Kukabidhi Zawadi kwa Shule tano za Sekondari zilizofanya vizuri katika matokeo ya Mtihani wa kidato cha nne mwaka 2016, Pamoja na Shule 5 za Msingi zilizofaulisha vizuri Mtihani wa Darasa la saba mwaka 2016.	Ilemba	0	Kiongozi wa mbio za Mwenge
	10:05- 11:55	**Risala ya Utii, Utambulisho, UJUMBE WA MWENGE(Uwanja wa Mpira Ilemba)**	Ilemba	0	DC, DED na Kiongozi wa Mbio za Mwenge
	11:55- 01:00	**Mapumziko, Kuchangia damu, na Upimaji wa hiari wa VVU na UKIMWI (Uwanja wa Mpira). Mkesha**	Ilemba	0	DC, DED na Kiongozi wa Mbio za Mwenge
	01:00- 02:00	Chakula cha Jioni (**Shule ya Sekondari Ilemba**)	Ilemba	0	DC Sumbawanga , DED Sumbawanga
JUMLA NDOGO KM				**109**	
TAREHE	**MUDA**	**SHUGHULI**	**MAHALI**	**KM**	**MHUSIKA**
11/4/2017	11:00- 11:30	**Chai ya Asubuhi (Shule ya Sekondari Ilemba)**	Ilemba	0	DC Sumbawanga , DED Sumbawanga
	11:30- 1:30	Mwenge kuondoka Ilemba kupitia Kalambanzite,Lusaka,Laela, Miangalua, Tunko na kuwasili eneo la	Ilemba	71	DC Sumbawanga , OCD

		makabidhiano Kijiji cha Mkutano Mkoa wa Songwe			
	1:30 - 2:30	DC Sumbawanga kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa RC RUKWA	Mkutano	0	DC Sumbawanga, RC RUKWA
	2:30 - 3:00	RC RUKWA kukabidhi Mwenge kwa RC SONGWE	Mkutano	0	RC RUKWA, RC SONGWE
JUMLA NDOGO KM				**71**	
JUMLA KUU KM				**180**	

TAARIFA FUPI YA KUKABIDHI MIZINGA KUMI (10) KIKUNDI CHA WAFUGAJI NYUKI CHA KIZUNGU NA JOZI TANO (5) ZA MAVAZI YA KURINIA ASALI KWA VIKUNDI VYA UFUGAJI NYUKI KUTOKA MUZE NA MFINGA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA, BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Katika kuitikia wito wa Taifa wa kuhifadhi mazingira, kijiji cha Kizungu kimetenga eneo la hifadhi ya msitu wenye ukubwa wa ekari 20 lililoanza kuhifadhiwa mwaka 2004. Kijiji kiliunda kikundi cha ufugaji wa nyuki chenye wanachama kumi na watatu (13) kati yao ke 5 na me 8 ambao ni wakazi wa kijiji hiki. Lengo ni kufuga nyuki ili kujiongezea kipato, kuacha uchomaji wa mkaa na kuhamasisha wananchi wengine kuhifadhi mazingira yanayowazunguka kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho. Halmashauri inatoa mizinga 10 ya kisasa pamoja na Jozi 5 za Mavazi ya kinga kwa Vikundi vitatu yenye thamani ya shilingi 1,336,000/=

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa heshima na taadhima tunakuomba ukabidhi mizinga kumi (10) ya nyuki na Jozi 2 kwa kikundi cha Kizungu, kisha ukabidhi jozi 2 kwa uongozi wa kikundi cha ufugaji nyuki cha MWENGE kutoka Mfinga na Jozi 1 Kikundi cha UMIUNYU kutoka Muze.

Ufugaji Nyuki katika Hifadhi ya Msitu wa Kijiji cha Kizungu – Kata ya Muze

MWENGE OYEE!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA KUWEKA JIWE LA MSINGI NYUMBA BORA YA MWANANCHI IDD MUSTAPHA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Mbele yako ni Mradi wa Ujenzi wa Nyumba Bora Vijijini, Mradi huu unamilikiwa na kuendeshwa na kijana anayeitwa Idd Mustapha mwenye umri wa miaka 31. Nyumba hii inatarajiwa kukamilika kwa gharama ya shilingi milioni mia moja, hadi ilipofikia sasa imetumia shilingi milioni 68,000,000/-. Nyumba hii itakuwa ya kibiashara ambayo ina vyumba 8, na anatarajia kupata shilingi 120,000/= kwa siku kwa bei ya chumba kimoja shilingi 15,000/=. Ambapo kwa mwaka anakisia kupata shilingi 43,200,000/= bila makato ya kodi na gharama za uendeshaji.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Nyumba hii inajengwa kwa awamu, kwa kutumia mapato yatokanayo na kilimo cha Mpunga na Mahindi ambapo mwaka 2016 alivuna na kuuza mazao na kupata jumla ya shilingi 25,000,000/= ambazo alizitumia kuendeleza ujenzi.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Kwa Heshima na taadhima tunaomba uweke jiwe la msingi nyumba hii ikiwa ni sehemu ya hamasa kwa vijana na wananchi wengine kuiga mfano huu wa kutumia mapato yatokanayo na shughuli zao za kilimo na ufugaji kujenga nyumba bora za kuishi na za Biashara vijijini

Ujenzi wa Nyumba Bora ya Mwananchi Muze

MWENGE OYEEEEE!!!!!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA UJENZI WA JENGO LA UTAWALA KATIKA SHULE YA SEKONDARI VUMA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Shule ya Sekondari ya Vuma ipo katika Kata ya Mtowisa, Tarafa ya Mtowisa, Shule hii ilifunguliwa mwaka 1998 na mpaka sasa ina jumla ya wanafunzi 422, kati yao wavulana 254 na wasichana 168, aidha shule hii ina jumla ya walimu 21, ikiwa wanaume 19 na wanawake 02. Shule hii itaanza kutoa Elimu ya kidato cha V na VI kuanzia mwezi Julai, 2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Ujenzi wa jengo la Utawala ulianza Oktoba, 2011 na upo katika hatua ya ukamilishaji. Mradi umegharimu jumla ya shilingi 22,238,500/= kati ya hizo Serikali kuu imechangia shilingi. 10,000,000/= na Wananchi wamechangia shilingi 12,238,500/=, hadi mradi ukamilike utagharimu shilingi 52,428,500/=.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Manufaa ya mradi utakapokamilika; utawapatia walimu ofisi na eneo la kutunzia vifaa vya kufundishia na kujifunzia hatimaye kuboresha huduma zitakazotolewa ambazo zitaongeza ufaulu wa wanafunzi.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa heshima na tahadhima tunakuomba uweke Jiwe la Msingi jengo la Utawala katika shule ya sekondari Vuma, Mradi huu ukwenda sambamba na ujenzi wa Madarasa 2 pamoja na ukarabati wa Hosteli na Bwalo la chakula na kwaajili ya kupokea kidato cha tano,2017. Ujenzi wa miundombinu umegharimu shilingi 132,381,450/= ikiwa wananchi wamechangia shilingi 18,000,000, Halmashauri shilingi 39,000,000/=,Serikali kuu shilingi 68,031,450/= na Mfuko wa Jimbo shilingi 7,3500,000 kwa ajili ya ununuzi wa vitanda 30 (Double Decker).

Ujenzi wa Jengo la Utawala Shule ya Sekondari Vuma - Kata ya Mtowisa

TAARIFA FUPI YA UJENZI WA CHUMBA KIMOJA CHA MAABARA YA KEMIA KATIKA SHULE YA SEKONDARI VUMA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA
BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Shule ya Sekondari ya Vuma ipo katika Kata ya Mtowisa, Tarafa ya Mtowisa, Shule hii ilifunguliwa mwaka 1998 na mpaka sasa ina jumla ya wanafunzi 422, ikiwa wavulana 254 na wasichana 168, aidha shule hii ina jumla ya walimu 21, ikiwa wanaume 19 na wanawake 02.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Ujenzi wa chumba kimoja cha maabara katika shule ya Sekondari Vuma ulianza Novemba, 2014 na kukamilika mwaka 2016. Mradi wa maabara umegharimu jumla ya shilingi 78,679,275/=, ikiwa ni fedha toka Serikali Kuu chini ya Mpango wa Maendeleo katika Shule za Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) na mchango wa wananchi ni eneo lililotumika kujenga maabara hiyo. Kukamilika wa ujenzi wa chumba cha maabara ya kemia utanufaisha wanafunzi 422, kwa kupata elimu ya sayansi kwa njia ya vitendo hivyo tunatarajia kupata wataalam wa sayansi wengi zaidi hapo baadaye.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Sasa tunakuomba uzindue chumba cha maabara ya kemia katika shule ya sekondari Vuma.

Ujenzi wa Chumba cha Maabara Shule ya Sekondari Vuma – Mtowisa

MWENGE OYEE!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA UHAWILISHAJI WA RUZUKU KWA KAYA MASIKINI CHINI YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (TASAF III), KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR
TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga inatekeleza Mpango wa kunusuru Kaya Masikini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF awamu ya tatu. Lengo kuu la Mpango huu ni kuziwezesha Kaya Masikini kumudu mahitaji muhimu ya Kaya ikiwa ni pamoja na kumudu huduma za Afya na Shule. Jumla ya Kaya Masikini **5199** zimenufaika na mpango huu, kuanzia Septemba 2015 hadi Machi 2017, jumla ya shilingi **2,113,824,400/=** zimehawilishwa katika Halmashauri katika Vijiji **65** na Mji mdogo wa Laela.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Kijiji cha Mtowisa ni miongoni mwa vijiji 65 na Mji Mdogo wa Laela vilivyonufaika na Mpango huu, kina jumla ya Walengwa **136,** hadi kufikia Machi 2017 jumla ya shilingi **49, 284,600/=** zimehawilishwa Kijijini hapa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Kwa heshima na taadhima tunaomba ukabidhi **VYETI** kwa Walengwa watano wa Kijiji cha Mtowisa ‘A’ ambao wameweza kutumia fedha ya **RUZUKU** waliyokuwa wakipokea kwa kuanzisha miradi midogo midogo ya Ufugaji wa nguruwe 22 mbuzi 3, shamba la mahindi ekari 4, shamba la mpunga ekari 1 na nyumba za kuishi zilizoezekwa kwa bati.

Wanufaika wa Mradi wa TASAF Kijiji cha Mtowisa ‘A’
MWENGE OYEEEEEEEEEEE!!

TAARIFA YA KUKABIDHI MIKOPO KWA VIKUNDI VYA VIJANA NA WANAWAKE VYA KAMPANI –KIFINGA, TUSAPE - MTOWISA NA LUNZA - ZIMBA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge Uhuru Kitaifa,

Vikundi vya vijana na wanawake vilivyotajwa hapo juu vimeanzishwa kwa nyakati tofauti na Vijnaa na wanawake wenyewe, kwa lengo la kukusanya mitaji ya ndani ili wakopeshane na waendeshe miradi ya vikundi. Vikundi hivi vina jumla ya wanachama 55 wakiwemo wanawake 33 na wanaume 21. Kati ya wanachama hao vijana ni asilimia 73 na waliobaki ni wanawake watu wazima, kuanzia miaka 36 – 49

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge Uhuru Kitaifa,

Halmashauri ya Wilaya kupitia Mfuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana imeamua kuunga mkono juhudi za vijana na wanawake hawa kwa kuwawezesha kiuchumi kwa kuwapa mikopo yenye riba nafuu ya 10% tu kwa mwaka.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge Uhuru Kitaifa,

Kwa Heshima na taadhima tunaomba ukabidhi hundi kwa viongozi wa vikundi hivi vitatu mkopo wa shilingi 6,300,000/= ikiwa kikundi cha Tusape shilingi 2,300,000/=, Kikundi cha Kampani shilingi 2,000,000/= na Kikundi cha Lunza shilingi 2,000,000/=

MWENGE OYEEEEE!!

TAARIFA FUPI YA SHAMBA LA ALIZETI LA NDUGU CHRISTOPHER DAUDI NYATO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10 /04/2017.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Mbele yako ni mradi wa shamba langu la Alizeti nililolima lenye jumla ya ekari 60. Shamba hili lilipandwa tarehe 17 – 18/02/2017 na aina ya mbegu iliyotumika ni Record. Gharama zilizotumika mpaka sasa ni shilingi 10,800,000/=.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Matarajio yangu ni kuvuna jumla ya gunia 500 zenye uzito wa kilo 60 kila moja, na Ninatarajia kuuza kwa shilingi 45,000/= kwa kila gunia, hivyo kupata jumla ya shilingi 22,500,000/=. Pamoja na shamba hili pia nimelima zao la Mahindi lenye ukubwa wa ekari 32 kwa Gharama ya shilingi 7,040,000/=. Ninatarajia kuvuna Gunia 300 ambazo nitauza kwa bei shilingi 50,000/= kwa kila gunia hivyo kupata jumla ya shilingi 15,000,000/=.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Matarajio yangu ya baadaye ni kununua trekta kwa ajili ya kulima zaidi ya hapa lengo ni hadi kufikia Ekari 200 za Alizeti na Mahindi, sambamba na hilo nategemea kununua mashine ya kusindika Alizeti ili kuongeza thamani ya Mazao yangu na kuongeza ajira kwa Wananchi na kuinua uchumi wa Halmashauri

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa Heshima na taadhima nakukaribisha ulione shamba langu.

Shamba la Alizeti Kijiji cha Zimba

MWENGE OYEEEEE!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU 6 KATIKA SHULE SEKONDARI MILENIA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Shule ya Sekondari Milenia ipo Kata ya Milepa, Tarafa ya Mtowisa, Shule hii ilifunguliwa mwaka 2009 na mpaka sasa ina wanafunzi 260, wavulana 145 na wasichana 115, aidha shule ina walimu 15, ikiwa wanaume 12 na wanawake 03.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Ujenzi wa nyumba ya Walimu 6 katika shule ya Sekondari Milenia ulianza mwaka 2016 na upo katika hatua ya ukamilishaji. Mpaka sasa umegharimu jumla ya shilingi 102,000,000/= ikiwa ni fedha toka Serikali Kuu chini ya Mpango wa Maendeleo katika Shule za Sekondari Awamu ya Pili (MMES II). Mpaka mradi ukamilike utagharimu shilingi 150,000,000/=, aidha Shule ina jumla ya Eneo lenye ukubwa wa Ekari 10 ambazo zilitolewa na Wananchi.

Kukamilika kwa ujenzi wa Nyumba hii kutapunguza tatizo la upungufu wa Nyumba za Walimu uliopo katika shule ya Sekondari ya Milenia pamoja na kuongeza uwajibikaji kwa Walimu.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa heshima na tahadhima tunakuomba uweke jiwe la msingi katika nyumba hii.

Ujenzi wa Nyumba ya Walimu 6 Shule ya Sekondari Milenia – Kata ya Milepa

MWENGE OYEE!!!!!!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA KLABU YA WAPINGA RUSHWA NA DAWA ZA KULEVYA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MILENIA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA
BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Mapambano dhidi ya rushwa na dawa za kulevya si ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa au Jeshi la Polisi peke yake bali ni jukumu la jamii nzima. Kwa kutambua hilo Halmashauri kwa kushirikiana na TAKUKURU na Jeshi la Polisi kupitia Idara ya Elimu kwa Umma inashirikisha jamii nzima katika mapambano haya, pamoja na wanafunzi waliopo shuleni kwa kuunda klabu za wapinga rushwa na dawa za kulevya. Shughuli za klabu ni pamoja na kuhamasisha jamii nzima katika mapambano dhidi ya rushwa na dawa za kulevya kwa njia ya Midahalo, Nyimbo, Ngonjera, Maigizo, Uandishi wa Insha na Uchoraji wa Katuni. Klabu ya wapinga Rushwa na madawa ya kulevya inaundwa na Wanafunzi wanachama wapatao 59 kati yao wavulana 38 na wasichana 21 wakiongozwa na mwalimu mlezi.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Lengo la kuunda klabu ya wapinga rushwa na dawa za kulevya katika shule ya Sekondari Milenia ni kuwafanya wanafunzi hao waelewe ubaya wa rushwa ili waichukie na kupambana nayo, na vilevile wajue madhara ya dawa za kulevya tangu wangali wadogo ili waepukane nayo na hatimaye kuwa na kizazi chenye nguvu kwa maendeleo ya Taifa. Pia kuwasadia watu walioathirika na dawa za kulevya kwa kuwaelekeza katika kliniki iliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa inayohudumia waathirika wa dawa za kulevya. Wananchi wa kata ya Milepa watanufaika kutokana na Elimu itakayotolewa na Klabu.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Sasa tunakuomba utuzindulie klabu ya Wapinga Rushwa na Dawa za Kulevya

MWENGE OYEE!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA UJENZI WA MADARASA 2 SHULE YA SEKONDARI MILENIA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Shule ya Sekondari Milenia ipo katika Kata ya Milepa, Tarafa ya Mtowisa, Shule hii ilifunguliwa mwaka 2009, mpaka sasa ina jumla ya wanafunzi 260 na walimu 15.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Ujenzi wa madarasa 2 shule ya Sekondari Milenia ulianza mwaka 2016 na upo katika hatua ya ukamilishaji. Ujenzi wa madarasa haya mawili umegharimu shilingi 49,404,075/= ikiwa ni fedha toka Serikali Kuu chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu katika Shule za Sekondari Awamu ya Pili (MMES II). Mpaka mradi ukamilike utagharimu shilingi 76,415,535/=.Mradi utawanufaisha
wanafunzi na walimu kwa kuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Kwa heshima na tahadhima tunakuomba utuweke jiwe la msingi katika madarasa haya.

-

Ujenzi wa Madarasa 2 Shule ya Sekondari Milenia - Kata ya Milepa

MWENGE OYEE!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA MRADI WA UFUGAJI SAMAKI KATIKA KIJIJI CHA MILEPA KATA YA MILEPA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Mradi wa Bwawa la ufugaji wa Samaki unamilikiwa na kikundi cha wafugaji samaki kijiji cha Milepa. Kikundi hiki kina jumla ya wanachama 16 ambapo wanaume ni 10 na wanawake 6. Mradi huu ulianzishwa rasmi mwaka 2015 na una ukubwa wa mita za mraba 13,020 ikiwa na urefu wa mita 140 na upana wa mita 93. Jumla ya samaki 29,499 walipandikizwa ikiwa 4,926 ni pelege na kambale 24,573. Lengo la mradi huu ni kuongeza uzalishaji kutoka 29,499 hadi kufikia 65,100 kwa mwaka. Bwawa hili ni miongoni mwa mabwawa matano yaliyopo katika Kijiji cha Milepa yenye ukubwa wa mita za mraba 14,344.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Ujenzi wa mradi huu una thamani ya shilling 19,214,400/= ikiwa shilingi 14,657,200 ni mchango wa Kikundi na shilingi 4,557,200/= mchango wa Mbunge wa Jimbo la Kwela Mhe: Ignas Malocha.

Uwepo wa mradi huu utasaidia upatikanaji wa samaki kwa urahisi zaidi chakula na kuboresha afya ya jamii, pia mradi huu utaongeza kipato kwa wananchi na kuboresha maisha yao. Aidha mradi utasaidia uhifadhi wa Ziwa Rukwa kwani utapunguza utegemezi wa Ziwa Rukwa hivyo kupunguza uvuvi haramu na kuongeza uhifadhi wa mazingira ya Ziwa (Buffer zone).

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa heshima na tahadhima tunaomba utuzindulie mradi huu.

Bwawa la Samaki la kikundi cha wafugaji wa samaki- Kijiji Cha Milepa

MWENGE OYEEEE!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA UJENZI WA ZAHANATI YA KIJIJI CHA KINAMBO KWA KIONGOZI WAMBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wambio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Mradi wa ujenzi wa jengo la Zahanati ulianza mwaka 2012/2013 kwa nguvu za Wananchi, gharama ya mradi mpaka utakapo kamilika utatumia shilingi 370,000,000/= kwa mchanganuo ufuatao:-.

1. Jengo la wagonjwa wa n je Tsh. 200,000,000/=
2. Samani pamoja na vifaa tiba Tsh. 100,000,000/=
3. Nyumba ya mtumishi Tsh. 70,000,000/=

JUMLA **TSH. 370,000,000**/=

Hadi kufikia hapo jengo lime gharimu kiasi cha shilingi 117,000,000/= kwa mchanganuo ufuatao.

1. Michango ya jamiii shilingi Tsh, 50,000,000/=
2. Michango wa Halmashauri shilingi Tsh, 67,000,000/=

JUMLA **TSH, 117,000,000/=**

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Baada ya Mradi huu kukamilika unatarajia kuhudumia wakazi 5,582 wa kijiji cha kinambo na Vijiji vya jirani.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa heshima na taadhima Tunakuomba utuwekee jiwe la Msingi.

Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji Cha Kinambo – Kata ya Milepa

MWENGE OYEEEE!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA MRADI WA MAJI KIJIJI CHA SOLOLA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Mradi wa Maji ya Msererekо Kijiji cha Solola ni Miongoni mwa Miradi 14 katika vijiji ambavyo vimepatiwa huduma ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kupitia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji **(WSDP).** Mradi huu ulianza kutekelezwa Februari 2015 na kukamilika Oktoba 2016 na Mkandarasi **Ms.FALLY ENTERPRISES LIMITED** kwa Gharama ya shs. 325,123,500/= ikiwa ni fedha toka Serikali Kuu, aidha wananchi kupitia Kijiji wametoa Ardhi ekari 10 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa Mradi.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kazi kuu zilizofanyika kwenye Mradi huu ni Ujenzi wa Kitovu cha maji “Intake”, utandazaji wa Bomba, ujenzi wa Tanki 75M^3 Ujenzi wa Vituo 12 na Uzio wa kuzunguka Tanki.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Mradi huu wa maji unanufaisha watu **2,703** wa Kijiji hiki na unategemewa kudumu kwa takribani miaka ishirini toka kukamilika wake. Kijij kimeunda chombo cha watumiaji maji, ambacho kitaendesha na kusimamia Mradi huu

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Kwa heshima na Taadhama, naomba utuzindulie Mradi huu, pia uwakabidhi Cheti Jumuia ya watumiaji maji Kijiji cha Solola.

Mradi wa Maji Kijiji Cha Solola – Kata ya Nankanga

MWENGE OYEEE!!!!!!!!!!!!!!!!!!,

TAARIFA FUPI YA UGAWAJI WA VYANDARUA KWA WAZEE, WAJAWAZITO NA WATOTO CHINI YA MIAKA MITANO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA
BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga inatambua kuwa ugonjwa wa malaria ni miongozi mwa magonjwa yanayosumbua watu wengi katika Halmashauri. Hivyo wataalam wameendelea kuhamasisha wananchi kutumia njia mbali mbali za kujikinga na ugonjwa huo ikiwemo matumizi sahihi ya vyandarua. Takwimu zinaonesha kuwa katika Halmashauri yetu waathirika walio wengi ni kundi la wajawazito, wazee na watototo chini ya miaka mitano.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
Halmashauri kwa kushirikiana na wananchI imeendelea kupambana ili kutokomeza ugonjwa wa Malaria, elimu kwa wananchi imetolewa juu ya kutokomeza mazaria ya Mbu na kuhakikisha usafi wa Mazingira unafanyika pamoja na kampeni ya kufanya usafi kila mwisho wa Mwezi . Aidha ili kuhakikisha ugonjwa wa Malaria unatokomezwa, katika kipindi cha hadi kufikia Machi 2017 Halmashauri imefanikiwa kugawa vyandarua 860 kwa wananchi vyenye thamani ya shilingi 6,020,000/=. Jitihada hizi na nyingine zimefanikisha kwa kiasi kikubwa kupunguza maambukizi ya malaria kwa 96% toka 80% mwaka 2015, wananchi wameendelea kuhimizwa kufika katika vituo vya kutolewa huduma za afya pindi wanapohisi dalili za ugonjwa wa malaria sambamba na kushauriwa kufuata ushauri wa Daktari kwa kutumia dawa za mseto iwapo watakutwa na ugonjwa wa malaria

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
kwa heshima na taadhima tunaomba uwagawie vyandarua 300 vyenye thamani ya shilingi 2,100,000/- wazee 5, akina mama wajawazito 5 na watoto 5 kwa niaba ya wengine,.

MWENGE OYEEEEEEE!!!!!!!!!!!!!!!

TAARIFA FUPI YA KUKABIDHI ZAWADI KWA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ZILIZOFANYA VIZURI KATIKA MTIHANI WA TAIFA MWAKA 2016 KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA BWANA AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 10/04/2017

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina jumla ya Shule za Msingi 103 na Shule za Sekondari 21, ikiwa Shule 15 za Sekondari ni za serikali na shule 6 ni za binafsi. Jumla ya wanafunzi wa shule za Msingi 4539 walifanya Mtihani wa Taifa wa kuhitimu Darasa la Saba Mwaka 2016, wakiwemo wavulana 2196 na wasichana 2345. Kwa upande wa Shule za Sekondari wanafunzi 846 walihitimu Kidato cha Nne wakiwemo wavulana 503 na wasichana 343.

Kati ya Wanafunzi 4539 waliohitimu Darasa la Saba, wanafunzi 2523 walifaulu mtihani, kati ya hao wavulana ni 1399 na wasichana ni 1124, sawa na asilimia 56 ya ufaulu, kwa ufauru huo Halmashauri ikishika nafasi ya 4 Kimkoa. Kwa upande wa Shule za sekondari kati ya wanafunzi 846 walihitimu kidato cha nne wanafunzi 600 walifaulu mtihani, kati ya hao wavulana walikwa 402 na wasichana 198 ikiwa ni asilimia 71 ya ufaulu na kushika nafasi ya 2 Kimkoa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Shule 5 za Msingi zilizofanya vizuri Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka 2016 na kupata wastani wa ufaulu kama ifuatavyo; Laela “B” (156%), Laela “A” (154%), Kizungu (142%), Mleche (141%) na Ntumbi (135%). Aidha, shule 5 za sekondari zilizofanya vizuri katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2016 ni Kaengesa Seminari (100%), Miangalua (82%), Unyiha (80%), Ilemba (76%) na Mzindakaya (73%).

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.
Kwa Heshima na taadhima tunaomba ukabidhi hundi ya shilingi 2,000,000/= kwa shule za Msingi na Sekondari zilizofanya vizuri Mtihani wa Taifa mwaka 2016, ikiwa ni sawa na shilingi 200,000/= kwa kila shule ili kuwapa motisha na kuwapongeza kwa kufaulisha.

MWENGE OYEEEE!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!

MUHTASARI WA THAMANI YA MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE MWAKA 2017 SEKTA ZA UMMA /BINAFSI HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

SEKTA	JINA LA MRADI	MAHALI	SERIKALI KUU	HALMASHAURI	WADAU/ASASI	WANANCHI	JUMLA	SHUGHULI
MALIASILI	Mradi wa ufugaji Nyuki Vikundi vya Kizungu, Mfinga na Muze	KIZUNGU	-	1,336,000	-	-	1,336,000	Kukabidhi Mizinga na Jozi za kurinia Asali
M/JAMII	Ujenzi wa nyumba bora ya Mwananchi	MUZE	-	-	68,000,000		68,000,000	Kuweka jiwe la Msingi
ELIMU SEKONDARI	Ujenzi wa jengo la Utawala pamoja na Miundombinu katika Shule ya Sekondari Vuma	MTOWISA	85,381,450	39,000,000	-	30,238,500	154,619,950	Kuweka jiwe la Msingi
ELIMU SEKONDARI	Ujenzi wa Maabara ya Kemia	MTOWISA	78,679,275	-	-	-	78,679,275	Kuzindua chumba cha Maabara
TASAF	Mradi wa TASAF	MTOWISA	49,284,600	-	-	-	49,284,600	Kugawa vyeti
M/JAMII	Utoaji wa Mkopo wa Shilingi 6,300,000/= kwa vikundi vitatu vya Vijana	MTOWISA	-	6,300,000	-	-	6,300,000	Kukabidhi hundi
KILIMO	Mradi wa Kilimo cha Alizeti	ZIMBA	-	-	10,800,000		10,800,000	Kutembelea Shamba
ELIMU SEKONDARI	Ujenzi wa nyumba za Walimu (SEDEP)	MILEPA	102,000,000	-	-	-	102,000,000	Kuweka jiwe la Msingi

SEKTA	JINA LA MRADI	MAHALI	SERIKALI KUU	HALMASHAURI	WADAU/ASASI	WANANCHI	JUMLA	SHUGHULI
ELIMU SEKONDARI	Kikundi cha kupinga madawa ya kulevya na Rushwa katika Shule ya Sekondari Milenia	MILEPA	-	-	-	-	-	Kuzindua Kikundi
ELIMU SEKONDARI	Ujenzi wa Madarasa 2 Shule ya Sekondari Milenia	Milepa	49,404,075	-	-	-	49,404,075	Kuweka Jiwe la Msingi
MIFUGO/ UVUVI	Ujenzi wa Bwawa la Samaki Kijiji cha Milepa	MILEPA	-	-	4,657,200	14,557,200	19,214,400	Kuzindua bwawa
AFYA	Ujenzi wa Zahanati ya Kinambo	MILEPA	67,000,000	-	1,000,000	50,000,000	118,000,000	Kuweka jiwe la Msingi
MAJI	Mradi wa maji katika kijiji cha Solola	NANKANGA -SOLOLA	325,123,500	0	-	-	325,123,500	Kuzindua Mradi wa Maji
AFYA	Mradi wa kugawa Vyandarua 300 kwa akina Mama Wajawazito, Watoto na Wazee	ILEMBA	-	2,100,000	-	-	2,100,000	Kukabidhi vyandalua
ELIMU	Kukabidhi zawadi kwa Shule tano za Sekondari zilizofanya vizuri katika Matokeo ya mtihani wa Kidato cha nne mwaka 2016, Pamoja na shule 5 za Msingi zilizofaulisha vizuri	ILEMBA	-	2,000,000	-	-	2,000,000	Kukabidhi zawadi
JUMLA KUU			**756,872,900**	**50,736,000**	**84,457,200**	**94,795,200**	**986,861,800**	


HALMASHAURI YA WILAYA SUMBAWANGA
RAMANI YA KUONESHA MIPAKA YA WILAYA
WILAYA YA MLELE
MFINGA
Kalambaleza
MUZE
Ilanga
Kizungu
Mkamba
MTOWISA
Zimba
ZIWA RUKWA
Msia
MANISPAA YA SUMBAWANGA
Kisa
Nankanga
MILEPA
MSANDAMUNGANO
SANDULULA
From Tamasenga
Mkunda
Sakalilo
ILEMBA
KAENGESA
Malolwa
KAOZE
Kilyamatundu
MPUI
KIPETA
KALAMBAZITE
Kizumbi
WILAYA YA KALAMBO
WILAYA YA MOMBA
LUSAKA
LAELA
Kisalala
MIANGALUA
Mititi
Tunko
TO MBEYA
407500
407750
408000
408250
408500
9039750
9039500
9039250
9039000
9038750
UFUNGUO
Barabara ya Miguu
Mpaka wa Wilaya
Barabara Kuu
Barabara za Wilaya
Hifadhi yaa Uwanda
Hifadhi ya Ziwa
Makazi
Hifadhi ya Milima ya Ufipa
Ziwa Rukwa
Kilimo
Scale
0 30 60 120 180 240